**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**

# KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA,UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 17/2/2022 KWA AJILI YA KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA MWEZI DESEMBA, 2021

*Imetayarishwa Na;*
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE**
**S.L.P. 686**
**MPANDA-KATAVI**

**FEBRUARI, 2022**



Scanned with CamScanner

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 16/12/2021 KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI KWA AJILI YA KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA MWEZI NOVEMBA, 2021

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

| NA | JINA | WADHIFA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe.Soud M.Mbogo | Mwenyekiti | Diwani Kata ya Inyonga & Mwenyekiti Halmashauri |
| 2. | Teresia A.Irafay | Katibu | Mkurugenzi Mtendaji |
| 3. | Mhe.Leonard A.Kiyungi | Mjumbe | Diwani Kata ya Kamsisi & Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri |
| 4. | Mhe.William V.Miula | Mjumbe | Diwani Kata ya Ilela |
| 5. | Mhe.Grace R.Kapalia | Mjumbe | Diwani Viti Maalum Kata ya Inyonga |
| 6. | Mhe.Martin J.Mgoloka | Mjumbe | Diwani Kata ya Ilunde |

**WAALIKWA**

| Na | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 01 | Lincoln B.Tamba | KATIBU TAWALA WILAYA YA MLELE |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA.**

| NA | JINA | WADHIFA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe.Isack Kamwelwe | Mjumbe | Mbunge wa Jimbo la Katavi |

**WATAALAMU**

| NA | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Hussein Lufulondama | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala |
| 2. | Obindi J.Wembe | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 3. | Norbert Magengele | Mkuu wa Kitengo cha Ugavi |
| 4. | Alfred R.Sungura | Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji |
| 5. | Dr.John Marco | Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya |
| 6. | Eng.Abdul Frank | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 7. | Ignas Kikwala | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 8. | Luke D.Kifyasi | Mkuu wa Idara ya Kilimo,Ushirika na Umwagiliaji |
| 9. | Gerald Gandye | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 10. | Hussein S.Msumi | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 11. | Gilbert E. Kasavila | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira |
| 12. | Joseph Sanga | Afisa Ushirika |



Scanned with CamScanner
CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Joseph P.Mkumbwa | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 14. | Timothy E.Bernard | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 15. | Paschal L.Berege | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |

**SEKRETARIETI**

| Na | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Daud J.Mwakagile | Mwandishi wa Vikao |

## AJENDA.NA.KTV/MLDC/1/12/ 2021: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 8 : 36 mchana.

## AJENDA.NA.KTV/MLDC/2/12/ 2021: KUSOMA NA KURIDHIA AJENDA

**Katibu** aliwasilisha ajenda kama ifuatavyo;

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuridhia ajenda
3. Taarifa za utekelezaji kwa idara na vitengo kwa mwezi Novemba,2021
   a. Idara ya Fedha na Biashara
   b. Idara ya Utawala na Utumishi
   c. Kitengo cha Ugavi
   d. Taarifa ya iCHF
   e. Kitengo cha Sheria
4. Taarifa ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya
5. Taarifa ya ujenzi wa jengo la Utawala
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi ya maendeleo
7. Maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19
8. Mpango wa ununuzi wa mashine kwa ajili ya ufyatuaji wa matofali ya block
9. Udhibiti wa virusi vya UVIKO – 19
10. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
11. Kufunga kikao



Scanned with CamScanner

mkandarasi mshauri Bureau for Industrial Cooperation (BICO) ambapo kazi zifuatazo zinaendelea:-

- Upigaji wa plasta
- Upigaji wa bati

Baada ya uwasilishaji huo hapakuwa na hoja.

**AJENDA.NA.KTV/MLDC/6/12/ 2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSH. 3,755,532,605.43**

Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ifuatayo;

Halmashauri katika kipindi cha mwezi Novemba na desemba imepokea fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi (**sh. 3,755,532,605.43**). Fedha hizi ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Afya (**sh 2,390,000,000.00**), Sekta ya Elimu idara ya elimu Msingi (**sh. 187,110,000.00**) Elimu Sekondari (**sh. 732,500,000.00**) na Utawala (**sh.445, 922,605.43**)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Katika mapokezi hayo zipo fedha zilizopokelewa nje ya Mpango na Bajeti na nyingine zimepokelewa kadri ya Mpango na Bajeti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Katika kipindi cha mwezi Novemba na Desemba fedha zilizopokelewa nje ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, Halmashauri imepokea kiasi cha kiasi cha sh. **1,110,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa miundo mbalimbali katika sekta za Elimu Sekondari na afya kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini:

**JEDWALI NO.1: FEDHA ZILIZOPOKELEWA NJE YA MPANGO NA BAJETI**

| Na | LENGO | CHANZO CHA FEDHA | BAJETI TENGWA (SH) | FEDHA ILIYOPOKELEWA (SH) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la dharura Hospitali ya Halmashauri | IMF | 0.00 | 300,000,000 |
| 2 | Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa afya 3 in 1 kituo cha afya cha Ilunde | IMF | 0.00 | 90,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa shule mpya ya kata Kamsisi | SEQUIP | 0.00 | 470,000,000 |
| 4 | Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) Kituo cha afya cha Ilunde | SERIKALI KUU/TOZO | 0.00 | 250,000,000 |
| JUMLA | | | **0.0** | **1,110,000,000** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Katika robo ya Kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele iliwasilisha Maombi ya Fedha kiasi cha sh. 2,199,610,350.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Afya na Elimu Msingi na Sekondari. Fedha zilizoombwa ni ruzuku ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoidhinishwa katika Mpango na Bajeti ya Halmashauri. Aidha fedha zilizoombwa



Scanned with CamScanner

zimeletwa kiasi cha shilingi 2,199,610,000.00 sawa na asilimia 99.99% ya fedha yote iliyoombwa. Kama invyooneshwa kwenye jedwali hapo chini;

| Na | SEKTA | BAJETI TENGWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|---|
| | Afya | 1,750,000,000.00 | 1,750,000,000.00 | 100 |
| 1 | Elimu - Msingi | 187,110,350.00 | 187,110,000.00 | 99.99 |
| 2 | Elimu - Sekondari | 262,500,000.00 | 262,500,000.00 | 100 |
| 3 | **JUMLA SH** | **2,199,610,350** | **2,199,610,000.00** | **99.99** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Mapokezi ya fedha hii itatekeleza miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mchanganuo ufuatao;

**A: SEKTA YA ELIMU – MSINGI**

| NA | JINA LA MRADI | KATA/KIJIJI | KIASI KILICHOID HINISWA | KIASI KILICHOPO KELEWA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule shikizi Ulyambogo | Ilunde/Isegene zya | 25,000,000 | 25,000,000 | Hatua ya lenta |
| 2 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Igombe | Inyonga/inyon ga | 24,610,350 | 24,610,000 | Chumba 1 hatua ya lenta |
| 3 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Kalovya | Inyonga/Kalov ya | 25,000,000 | 25,000,000 | Umaliziaji wa boma |
| 4 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Imalauduki | Kamsisi/Imala uduki | 25,000,000 | 25,000,000 | Umaliziaji |
| 5 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Motomoto | Ilela/Mapili | 25,000,000 | 25,000,000 | Saruji ya kufyatua ipo, kwa sasa ni mandalizi ya kazi |
| 6 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule shikizi Izenga | Utenda/Utende | 12,500,000 | 12,500,000 | Jengo limepauliw a |
| 7 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Kafulu | Utenda/Utende | 25,000,000 | 25,000,000 | Vyumba 2 vya madarasa na ofisi vimepauli wa. Hatua ya umaliziaji |
| 8 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya | Nsenkwa/Nsen | 25,000,000 | 25,000,000 | Hatua ya |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | madarasa shule ya msingi Nsenkwa | kwa | | | Lenta |
| **JUMLA** | | | **187,110,350** | **187,110,000** | |

**B: ELIMU SEKONDARI**

| NA | JINA LA MRADI | KATA/KIJIJI | KIASI KILICHOIDHINISWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | HATUA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Umaliziaji wa vyumba 3 vya madarasa shule ya sekondari Ilunde | Ilunde/Ilunde | 37,500,000 | 37,500,000 | Mradi haujaanza |
| 2 | Umaliziaji wa vyumba 3 vya madarasa shule ya sekondari Inyonga | Inyonga/inyonga | 37,500,000 | 37,500,000 | Vyumba 2 hatua ya umaliziaji na chumba 1 hatua ya ujenzi wa msingi |
| 3 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya sekondari Kamalampaka | Inyonga/Kamalampaka | 25,000,000 | 25,000,000 | Chumba 1 hatua ya lenta na kimoja hakijaanza kujengwa |
| 4 | Umaliziaji wa vyumba 3 vya madarasa shule ya sekondari Kamsisi | Kamsisi/Kamsisi | 25,000,000 | 25,000,000 | Vyumba viko hatua ya umaliziaji |
| 6 | Umaliziaji wa vyumba 3 vya madarasa shule ya sekondari Uzega | Utende/Utende | 37,500,000 | 37,500,000 | Boma la vyumba limekamilika |
| 7 | Umaliziaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya sekondari Isack Kamwelwe | Nsenkwa/Nsenkwa | 25,000,000 | 25,000,000 | Boma limekamilika, umaliziaji mwingine ulioendelea umefanyika kwa mkopo wa fedha za mapato ya ndani. |
| 8 | Ujenzi wa vyumba 3 vya maabara za masomo ya sayansi katika shule mpya za sekondari: | ~~Kamsisi/Kamaisis~~ | 75,000,000 | 75,000,000 | Mandalizi ya kazi |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kamsisi (1), Kamalampaka (1) na Uzega (1) | ~~Inyonga~~/Kamal ~~ampaka~~ Utende/~~utende~~ | | | |
| JUMLA | | | 262,500,000 | 262,500,000 | |

C: SEKTA YA AFYA

| NA | JINA LA MRADI | KATA/KIJIJI | KIASI KILICHOIDHINISWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi/Ukarabati Mkubwa wa zahanati kijiji cha Ipwaga | Ilela/Ipwaga | 100,000,000 | 100,000,000 | Mandalizi ya kazi |
| 2 | Ujenzi wa nyumba ya mganga, chomeo la taka, matundu ya vyoo na umaliziaji wa zahanati kijiji cha Kamalampaka | Inyonga/Kamalampaka | 50,000,000 | 50,000,000 | Mandalizi ya kazi. |
| 3 | Ujenzi wa wodi za wagonjwa (wodi ya upasuaji wa wanaume na wanawake, wodi ya daraja la kwanza na jengo la upasuaji) Hospitali ya Halmashauri | Inyonga/Inyonga | 800,000,000 | 800,000,000 | Mandalizi ya kazi |
| 4 | Ujenzi wa jengo la wagonjwa wan je (OPD), wagonjwa wa ndani (IPD) kwa ajili ya akina mama, wanaume na watoto Kituo cha Afya Ilunde | Ilunde/Ilunde | 400,000,000 | 400,000,000 | Mandalizi ya kazi |
| 6 | Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), kliniki ya Afya ya uzazi (RCH), maabara na jengo la mionzi | Kituo cha Afya Inyonga "B" | 400,000,000 | 400,000,000 | Mandalizi ya kazi |
| | **JUMLA** | | **1,750,000,000** | **1,750,000,000** | |

Sambamba na mapokezi ya fedha za sekta ya Afya Sekta ya Elimu msingi na sekondari, Halmashauri imepokea kiasi ch a shilingi **Sh. 445, 922,605.43** kama ilivyombwa kwa ajili ya muendelezo wa ujenzi wa jengo la Utawala ghorofa moja unaotekelezwa na Makandarasi Mjenzi SUMA-JKT Kanda ya Magharibi na Mkandarasi mshauri Bureau For Industrial Cooperation BICO) kutoka chuo kikuu cha Dar es Salaam. Mapokezi ya fedha hizi yatasaidia kuendelea na umaliziaji wa mradi huu.

Baada ya uwasilishaji huo yalifuata majadiliano kama ifuatavyo;

- Mhe.Leonard Kiyungi alitoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa fedha zilizo nje na bajeti,alishauri kuwa usimamizi wa matumizi ya fedha uwe kama ilivyokuwa katika fedha za UVIKO 19 awamu ya kwanza.
- Mhe.Martin Mgoloka alitoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa fedha zilizo nje na bajeti,alishauri kuwa usimamizi wa matumizi ya fedha uwe kama ilivyokuwa



Scanned with CamScanner

katika fedha za UVIKO 19 awamu ya kwanza na bajeti zijazo Mkurugenzi Mtendaji awasimamie Wakuu wa Idara na Vitengo kufahamu mahitaji halisi ya kila kata kupitia fursa na vikwazo.

- Katibu alieleza kuwa fedha za UVIKO – 19 awamu ya pili kwa upande wa afya miradi itatekelezwa kwa kandarasi,fedha nyingine zimetolewa bila maelekezo hata hivo matumizi yatatetekelezwa kwa kuzingatia taratibu na sheria.
- Mhe.William Miula alitoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa fedha zilizo nje na bajeti na kushauri kuwa Tsh.450,000,000 zilizotolewa Kamsisi zitumike kuendelelza ujenzi wa shule mama ya sekondari kuliko kuanzisha ujenzi wa shule nyingine ya sekondari.
- Mhe.Grace Kapalia alitoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa fedha zilizo nje na bajeti.
- Mhe.Martin Mgoloka alishauri kuwa ni vema ukatolewa muongozo wa matumizi ya fedha Tsh.450,000,000 zilizotolewa Kamsisi kwa ajili ya ujenzi wa sekondari.
- Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari alieleza kuwa ni vyema zikajengwa shule mbili za sekondari Kata ya Kamsisi ambapo moja itakuwa ni kwa masomo ya kidato cha sita kwani uwepo wa shule nyingi za sekondari unasaidia kuongezeka kwa bajeti ya elimu kiwilaya.Hivyo ni vyema Tsh.450,000,000 zikatumika kama zilivyotolewa na serikali katika ujenzi wa shule mpya ya sekondari kwa manufaa ya baadae,pia jitihada za ukamilishaji shule mama ziendelee.
- Katibu alitoa pongezi kwa Wataalam katika usimamizi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kwa fedha za UVIKO – 19.
- Mhe.Martin Mgoloka alishauri kuwa Wataalamu wafanye tathimini ya ukamilishaji ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Isack Kamwelwe ili kuwezesha urejeshwaji wa fedha iliyoazimwa.

Azimio

Wajumbe walikubaliana mambo yafuatayo;

- Tsh.470,000,000 zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Kamsisi zitumike kama zilivyotolewa ambapo shule ya ijengwe katika eneo ambalo awali lilitolewa na Serikali ya Kijiji kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Wasichana Kitongoji cha Shama.Taratibu ziendelee za ukamilishaji ujenzi wa shule ya sekondari inayojengwa kwa nguvu za wananchi.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 30,ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati na majengo ya vituo vya Afya utekelezwe kwa njia ya force account isipokuwa utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya Afya kupitia fedha za UVIKO – 19 Il ufanyike kupitia kandarasi kwa kuzingatia miongozo na maelekezo yaliyotolewa na Serikali.

**AJENDA.NA.KTV/MLDC/7/12/ 2021: MAENDELEO YA UTEKELEZAJI MIRADI INAYOTEKELEZWA KUPITIA FEDHA ZA UVIKO – 19**

Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ifuatayo;



Scanned with CamScanner

| JINA LA MRADI | JINA LA KITUO/SHULE | IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPOKELEWA | KIASI KILICHOTUMIKA | KIASI KILICHOBAKI | ASILIMIA YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Shule ya Sekondari Inyonga | SHULE YA SEKONDARI INYONGA | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 | 46,089,609.00 | 13,910,391.00 | 77% |
| Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Ilela | SHULE YA SEKONDARI ILELA | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 30,325,541.00 | 9,674,459.00 | 76% |
| Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Kamsisi | SHULE YA SEKONDARI KAMSISI | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 28,960,658.00 | 11,039,342.00 | 72% |
| Ujenzi wa chumba 1 vya madarasa Shule Sekondari Ilunde | SHULE YA SEKONDARI IILUNDE | 1 | 20,000,000 | 20,000,000 | 15,646,194.00 | 4,353,806.00 | 78% |



Scanned with CamScanner

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Utende | SHULE YA SEKONDARI UTENDE | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 29,424,891.00 | 10,575,109.00 | 74% |
| | JUMLA SEKONDARI | 18 | 200,000,000.00 | 200,000,000.00 | 150,446,893.00 | 49,553,107.00 | 75% |

Baada ya uwasilishaji huo yalifuata majadiliano kama ifuatavyo;

- Mhe.Martin Mgoloka alitoa pongezi kwa Wataalamu,Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya na Mkuu wa Wilaya katika usimamizi wa miradi.Mbinu zilizotumiwa katika usimamazi na utekelezaji wa miradi ziwe endelevu.

Baada ya majadiliano hayo Wajumbe waliridhia taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa .

**AJENDA.NA.KTV/MLDC/8/12/ 2021: MPANGO WA UNUNUZI WA MASHINE KWA AJILI YA UFYATUAJI WA MATOFALI YA BLOCK**

Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa kama ifuatavyo;
Naomba kuwasilisha katika kikao chako cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe **16/12/2021** ombi la kubadili matumizi ya fedha kiasi cha sh. 20,000,000 zilizolengwa kuendeleza stendi ya magari ya mizigo ili zitumike kununua mashine ya kufyatua tofali

Ombi hili linalenga kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo ununuzi wa mashine hii utawezesha mambo yafuatayo

i. Kuhakikisha kuwa Halmashauri inakuwa na benki ya tofali wakati wote hali itakayoharakisha kuanza na kukamilisha ujenzi wa miradi inayopokea fedha kwa wakati
ii. Kuhakikisha tofali zinapatikana kwa gharama nafuu ukilinganisha na kununua kutoka kwa wazabuni.
iii. Kuhakikisha kuwa Halmashauri inatekeleza miradi kwa kutumia tofali zenye viwango vinavyokubalika kitaalam
iv. Kuwa na mradi wa kimkakati (economic project) ikiwa ni hatua muhimu kuelekea kwenye kiwanda kidogo cha kufayatua tofali kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje

Maamuzi haya yametokana na mafanikio makubwa tuliyoyapata katika ujenzi wa vyumba 34 vya madarasa ambavyo vimetumia muda wa siku 49 kujengwa kuanzia tarehe 28/10/2021 hadi tarehe 15/12/2021. Uwepo wa tofali zilizokopwa shule ya



Scanned with CamScanner

CamScanner

| JUMLA | 3,569 | 2,439 | 290 | 39 |
|---|---|---|---|---|

I. HUDUMA ZA UPIMAJI

Hakuna mhisiwa wa ugonjwa wa uviko 19 aliyepatikana katika kipindi cha mwezi novemba kama ilivyo kwenye jedwali:-

| Jumla ya wahisiwa | Jumla ya sampuli zilizochukuliwa | Majibu yaliyorudi | Waliokua na majibu chanya | Waliokua na majibu hasi |
|---|---|---|---|---|
| 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

Baada ya uwasilishaji huo yalifuata majadiliano kama ifuatavyo;

- Mhe.William Miula alishauri kuwa hamasa ya chanjo iendelee kutolewa kwa wananchi.
- Mhe.Soud Mbogo alihoji endapo chanjo zinapatikana katika vituo vyote, Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya alieleza kuwa chanjo zinapatikana zahanati,Vituo vya Afya na Hospitali ya Wilaya
- Katibu alieleza kuwa timu ya idara ya afya itaendelea kuimarishwa kutoa chanjo ya UVIKO – 19 kwa kushirikiana na idara ya maendeleo ya Jamii.
- Mhe.Soud Mbogo alihoji kuwa chanjo ya pili ya sinopharm inatolewa baada ya siku ngapi, Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya alieleza kuwa chanjo ya pili utolewa baada ya siku 21.

**AJENDA.NA.KTV/MLDC/10/12/ 2021: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hapakuwa na mengineyo.

**AJENDA.NA.KTV/MLDC/11/12/ 2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 12 : 04 jioni.

**Muhtasari huu umethibitishwa na kusainiwa na;**

............................ ............................

**SOUD M.MBOGO** **TERESIA A.IRAFAY**

**MWENYEKITI** **KATIBU**

**TAREHE .17/3./2022**



Scanned with CamScanner

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA,UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 16/12/2021 KILICHOJADILI NA KUPITIA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA MWEZI NOVEMBA, 2021**

| AGENDA NA | AZIMIO/AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| TV/MLDC/8/12/ 2021 | **Azimio kwamba;**<br>• Tsh 470.000.000 zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Kamsisi zitumike kama zilivyotolewa ambapo shule ijengwe katika eneo ambalo awali lilitolewa na Serikali ya Kijiji kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya Wasichana Kitongoji cha Shama.Taratibu ziendelee za ukamilishaji ujenzi wa shule ya sekondari inayojengwa kwa nguvu za wananchi | DED | Azimio limetekelezwa Tsh 470.000.000 zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Kamsisi zinatumika kama zilivyotolewa ambapo shule itajengwa katika eneo ambalo limetolewa na Serikali ya Kijiji lililopo Kitongoji cha Shama , ambapo kwa sasa hatua ya usafishajiwa eneo unaendelea kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi. |
| | **Azimio kwamba**<br>• Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 30,ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati na majengo ya vituo vya Afya utekelezwe kwa njia ya force account isipokuwa utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya Afya kupitia fedha za UVIKO – 19 ili ufanyike kupitia kandarasi kwa kuzingatia miongozo na maelekezo yaliyotolewa na Serikali. | DED | Azimio limetekelezwa ambapo ukamilishaji wa majengo ya madarasa na zahanati pamoja na vituo vya afya unatekelezwa kwa force account.<br>utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya Afya kupitia fedha za UVIKO – 19 ili imeelekezwa kutekelezwa kwa njia ya force account badala ya kandarasi. |
| TV/MLDC/8/12/ 2021 | **Azimio kwamba;**<br>• Wajumbe waliridhia ununuzi wa mashine yenye thamani ya Tsh 27,000,000 kwa ajili ya ufyatuaji wa tofali za block ,utekelezaji ufanyike kwa | DED | Mashine imenunuliwa na imeanza kufanya kazi ya ufyatuaji wa tofali. |



Scanned with CamScanner

CamScanner

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wakati ili kurahisisha utekelezaji unaoendelea wa miradi ya maendeleo pamoja na kuwezesha kuongeza pato la Halmashauri. | | |



Scanned with CamScanner

CamScanner